

KRISTO NDANI YAKO

*Wakolosai 1:26 –29 “Ambao Mungu alipenda kuwajulisha
Jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii
katika mataifa, nao ni Kristo ndani yenu,
tumaini la utukufu”*

Natuangalie kile Nabii wa Mungu wa siku zetu alivyosema juu ya hilo:
“Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mnaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, na kuwa ndani yenu, hata mwisho wa wakati. “(Yohana Mt. 14:19-20) Kristo katika hori la ng’ombe? Hapana. Kristo ndani yako. Halleluya. Hatumuabudu Kristo aliye kwenye hori la ng’ombe, lakini ni Kristo ndani yako, Roho Mtakatifu, tumaini la maisha (Halleluya), muumbaji, Mungu mwenyewe alikaa ndani ya mwanadamu. “wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini tutamuona kama alivyo” (1Yohana 3:2). Kwa maana tutafanana naye.... Na kaka, dada, Huo Uungu uko ndani yako [1].

Msidanganyike, ni afadhali uchunguze hili kwa karibu sasa. Unaona, kama utaendelea kusema” Vema, hainihukumu mimi kufanya hivi na hainihukumu mimi kufanya hivi” mambo ya dunia? Sasa nitaenda kuwaumiza kidogo, tusukume manyoya Nyuma upande wa mwingine. Lakini huo ni ushahidi wa uhakika kwamba, hujawahi kukutana na Kristo, hujazaliwa mara ya pili. “Yeye aipendaye dunia au mambo ya dunia, upendo wa Mungu hauko ndani yake” (1Yoh. 2:15-17).

Sasa, kama unaacha kufanya hivyo kwa sababu unajua hupaswi kufanya hivyo, hiyo ni ishara ya kwamba hujafika popote bado. Wakati hicho kitu kinapokuwa kimekufa ndani yako, na asili yake imeondoka, hapo sasa kuna mtu mwingine pale.

Na itaweza tu kuzaa Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani ya Kristo akiwa ndani yako ataleta maisha yale yanayofanana na Kristo. Hakuna unachofanya;

Ni kile alichofanya. Alichagua hilo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu (Waefeso 1:3-4).

Mtu mmoja alisema, “Vema ninajua nimeokoka kwa kuwa nimeacha kuvuta”. Hiyo siyo sababu iliyonifanya niokoke, hiyo siyo sababu iliyokuacha uokolewe. Umeokolewa kwa sababu Mungu alikujua kabla ya kuwekwa misingi ya dunia ili uokolewe.

Hayo ni mafundisho ya kimaandiko. Amina. Sasa, unaona, tunaanza kuona kwamba, siyo sisi, ni yeye ametuchagua sisi (2Tim 1:9-10) [2].

“Vema mimi ni wa kanisa la Katoliki.” Hilo bado halimaanishi wewe ni Mkristo. Kuwa wa kanisa la Kibaptisti au Kimethodist haikufanyi wewe kuwa Mkristo. Kuna njia moja tu ya wewe kuwa mkristo. Neno “mkristo” Maana yake ni “Kuwa kama Kristo”. Na huwezi kulifanya hilo; huwezi ukalitendea kazi mwenyewe; hakuna njia hata kidogo uwezayo kulifanya hilo. Unapaswa ujisahau mwenyewe, ufe katika tabia zako, na umruhusu Kristo aje ndani yako na aishi maisha ya Kristo ndani yako [3].

Na njia pekee ambayo Mungu aweza kuhubiri injili leo ni kupitia ile taa ya udongo wa mfinyanzi, na ndiyo maana anakuweka wewe hapa. Na ndiyo maana ninyi watu wagonjwa mnayo haki ya kuja kwa Kristo. Nakusema, “Bwana Yesu, kama utaniponya mimi sasa, nitaenda. Ninaweza nisiwe mhubiri, lakini nitazungumza juu ya hilo. Nitafanya kila kitu niwezacho. Wewe ni mzabibu, mimi ni moja ya matawi”.

Sasa mzabibu hauzai matunda. Matawi ndiyo yanayozaa matunda, sio mzabibu, ni matawi. Mzabibu unatia nguvu tu kwa matawi Injili itahubiriwa na Kristo kama utafungua mwenyewe na uwe tawi ambalo litazaa matunda. Wengine watamwona Kristo ndani yako kwa ushuhuda wako, kwa maisha yako, na kwa jinsi

unavyoishi. Yeye ni nguvu, lakini wewe ndiyo picha inayo onyesha. Ni Biblia inayotembea (Yohana. 15:1-7) [4].

Naye alitembea nje akiwa amejibadilisha. Aliwatokea katika umbile la mtu (Luka 24:13-16) Anaweza akakutokea katika umbile la jirani yako. Anaweza akukutokea katika umbile la mhubiri au mama yako. Kristo anakutokea kupitia watu. Hivyo umfanyie kila mtu vyema kuwa mkarimu; kuwa Jirani mwema. Kuwa mwenye upendo. Kristo yuko ndani ya huyu mtu, “Kristo ndani yako tumaini la utukufu” (Wakolosai 1:26-27). Na kadri unavyoendelea mbele na watu wanakutokea, mtu mkarimu anaanza kuzungumza na wewe, wasikilize. Hujui, inaweza ikawa ni Yesu anayezungumza na wewe. Unaona, inatokea. Nitakuwa pamoja nanyi, na hata ndani yenu. Na kwa kadri ulivyowatendea hawa ulimtendea mimi (Matayo 25:40).

Oh unapoenda kuliangalia kwa njia hiyo, zile kanuni za zamani zinaanguka chini. Unaona? Haiwi ni mfumo wa maneno na utangazaji wa maneno yaliyokusanywa pamoja. Inakuwa ni urahisi wa Kristo aliye hai ambaye yuko ndani yetu sasa, Roho Mtakatifu akitembea mbele na nyuma, ndani ya kila Mwanadamu, akiingia ndani ya moyo, akichunguza, na kuhukumu maisha yaliyo haribika pale pale unapotubu, Anayashikilia mbele za Mungu, na Damu inakuosha Amina [5].

Unapovuka Yordani, Ni kifo; unaingia ndani ya pazia hilo nililokuwa ninazungumzia usiku uliopita, ndani ya patakatifu pa patakatifu mahali ambapo nuru yako siyo ya ulimwengu. Unatembea katika ushirika pamoja na Kristo aliye ndani yako, Yeye aliyetumaini la utukufu, Roho Mtakatifu akitembea na kuishi ndani ya mwanadamu anayekufa.

Na kama ningewaambia usiku wa leo, kwamba roho ya msanii mkubwa iko ndani yangu, utategemea nichore picha kama msanii. Kama ningekuambia kwamba roho ya John Dillinger ilikuwa ndani yangu, ungeniangua kuwa niwe na bunduki kubwa, na niwe mtu jasiri aliyetayari kufanya lolote, na kama nimekuambia Roho wa Kristo yuko ndani yangu, lazima nizifanye kazi za Kristo.

Na kama unakiri kuwa Mkristo, achana na dhambi na ubinafsi na hasira na uishi kama Kristo alivyofanya, maisha ya amani, unyenyekevu, yaliyobarikiwa na Mungu. Amina. Hiyo ni kweli [6].

Paulo alisema, “kwangu mimi kuishi ni Kristo na kufa faida” (wafilipi 1:21). “Siyo mimi niishiye tena, lakini ni Kristo akaaye ndani yangu. (Wagalatia 2:19-20) Kristo akiishi ndani ya mtu binafsi aliyesalimisha – nafsi yake. Kristo akizungumza kupitia midomo ya mtu binafsi akifikiri kupitia akili, akiona kupitia macho, akitenda kupitia tabia yako. Halleluya.

Hapo sasa mambo ya dunia yamepita. Itakuwaje kiti kingine ila utamu na ya kupendeza wakati wote? Kristo anatawala. Amina Unaliona hilo? Hivyo ndivyo ilivyo. Ni Kristo ndani yako. Kristo ndani yako [7].

Kama ningekuambia kwamba Roho wa Kristo yuko ndani yangu, hapo sasa Roho wa Kristo lazima atende sawa na alivyotenda ndani ya Kristo. Kama siyo, hapo sasa Roho wa Kristo haniongozi mimi. Ninaongozwa na Roho nyingine. Lakini kama Roho wa Kristo yuko ndani yako, hapo sasa uko kama Kristo, unakuwa mwanafunzi wa Kristo.

Na hapa ndipo watu leo huangalia misisimko mbalimbali ya kupiga kelele na kujiunga na kanisa na vitu kama hivyo, kuchukua mahali, au Elimu, au dhehebu, au kitu cha aina hiyo, kuchukua mahali pa Ukristo. Haitawezekana kamwe kuchukua mahali, haiwezi kufanya hivyo, Ni kristo ndani yako, tumaini la utukufu [8].

Miaka mingi iliyopita kabla hawajawa na vyombo vya kuyeyushia, walikuwa wanachukua dhahabu, na jinsi walivyojua kama ilikuwa sahihi au la, pamoja na takataka iliyotolewa ndani yake, mchanganyiko wote wa chuma (uitwao dhahabu ya mjinga).

Ujinga wote ulitolewa ndani yake, wapigaji waliipiga na kuipiga na kuigeuza na kuipiga na kuigeuza mpaka wapigaji waliona sura zao ndani ya ile dhahabu.

Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo kwa kanisa lake. Anakupa wewe jaribu baada ya jaribu, mtihani baada ya mtihani, jaribu baada ya jaribu, mtihani baada ya mtihani, mpaka maisha ya Kristo ya dhihirishwe katika maisha yako, mpaka unakuwa na amani, utulivu, mpole, mtu mwema, mnyenyekevu, aliyetayari, mvumilivu aliyetayari, kugeuza kichwa chake kutoka kwenye mambo ya dunia na kuangalia moja kwa moja msalabani kwa yule mmoja anayepiga.

Mara nyingi unafikiri ni mageni kwa sababu ya majaribu, na magonjwa na mateso (Rum 5:1-5), IPetro 4:12-13); yanafanyika tu kukujaribu wewe, kutoa uchafu ndani yako, kutoa takataka ndani yako, kutoa ulegevu (kwenda polepole) ndani yako, kukuamsha wewe kufikia mahali ambapo utaangalia na kumuona au watu waweze kumwona Kristo ndani yako: Kristo ndani yako, tumaini la utukufu [9].

Usijaribu kutafuta msisimko wowote, kitu chochote cha kuchukua mahali pa Roho Mtakatifu. Kule kuzaliwa kwa pili kunapokuja, wewe unabadilishwa. Huhitaji kufanya jambo lolote kuthibitisha hilo; Maisha yako yanalithibitisha hilo kwa jinsi unavyoenenda, upendo wako, Amani, Uvumilivu, upole, utuwema, subira, hivyo ndivyo ulivyo. Na dunia yote inaona udhihirisho wa Yesu Kristo ndani yako.

Sasa, kuzungumza kwa lugha, kupiga kelele pale, hivyo ni vitu tu vinavyofuatana na maisha ya aina hiyo. Na unaweza ukachukua na ukaigiza vitu hivyo na bado huna hayo maisha. Tunaona hayo. Ni wangapi wanajua kwamba hayo ni kweli? Hakika mnajua; ndiyo mnajua. Kwa nini unaweza ukayaona hayo kila mahali.

Kwa hiyo hakuna uwezacho kusema ni ushahidi wa kupokea Roho Mtakatifu, mpaka maisha yako unayoishi: sasa kama unataka kunena kwa lugha, hiyo ni nzuri kabisa kama unaishi

maisha ya kukuthibitisha katika hilo. Hiyo ni kweli. Na kama unataka kupiga kelele sawa ni vizuri, na piga kelele pia mara nyingine nafurahi sana mpaka nashindwa kuvaa hata viatu; nataka niruke nitoke ndani yake, na hilo ni la ajabu sana. Naliadini.

Na nimeona maono, na wagonjwa wanaponywa, wafu wanafufuliwa, wakati wamelala pale na daktari anaondoka na kusema imekwisha na hawaponi, nakaa hapo kwa masaa kadhaa; na Roho Mtakatifu anakuja pale na anaonyesha maono, na ninaenda pale na kumuamsha yule mtu. Nimeona wale walio viziwi, mabubu, na vipofu, na viwete, wakitembea. Haya hayafanyi..... hayo yote ni madhihirisho tu. [10].

Oh, jinsi Mungu anavyopenda kulibariki kanisa. Ni mara nyingi amewapaparikia ninyi, kama kuku afanyavyo vifaranga vyake, lakini hamkusikia. Mmesikiliza Viongozi wanadamu badala ya kiongozi Roho Mtakatifu mmesikiliza waalimu wanadamu badala ya mwalimu wa Mungu-Roho Mtakatifu, ambaye angewafundisha ninyi tabia, akiwafanya muwe na mwenendo safi, awafanye muwe wadada kweli, awafanye muwe chumvi ya dunia (Matayo 5:13).

Chumvi husababisha kiu. Na watu watatamani kuwa kama ninyi kama mtaishi kweli maisha ya Ukristo. Huwezi ukalifanya hilo wewe mwenyewe; lazima uwe na Kristo ndani yako kulifanya hilo. Dunia inahitaji kitu fulani halisi. Hiyo ndiyo sababu wanawaona watu wanaodai kitu fulani na kutoka nje na kufanya mambo kama wengine wote wa dunia [11]

Sasa, ule mti mdogo uko kama wewe, Baada ya kumkubali Kristo katika hali ya udogo wa mtoto (IYohana 2:12-13), Hapo tumepandwa pamoja ndani ya Kristo (1Kor 1:30-31). Sasa, kitu pekee huu mti mdogo unachofanya, unatakiwa tu kuumwagia maji, nao unaanza kunywa. Na unakunywa fungu lake ulilowekewa, lazima unywe zaidi ya hapo. Unakunywa sana mpaka unaanza kutoa matawi. Halafu unaendelea kunywa mpaka unatoa majani. Halafu unaendelea kunywa mpaka unatoa maua. Halafu unaendelea kunywa mpaka unatoa machungwa. Wakati wote unakunywa, unakunywa, unakunywa.

Na tunapokuwa watumishi wa Mungu waliozaliwa mara ya pili, mbegu ya Mungu imepandwa ndani ya mioyo yetu, tunaendelea kunywa, kunywa, na kukua.

Kila kitu unachokihitaji katika safari ya hapa duniani kiko ndani yako unapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Uponyaji wote uliowahi kuhitaji, kufurahi kote ambako ungehitaji, nguvu zote ulizowahi kuhitaji, kila kitu unachokihitaji kiko ndani yako unapokuwa na Kristo ndani yako (Yohana 10:10) lakini jambo moja linalokupasa kufanya ni kuendelea kunywa, kunywa.

Watu hawapati kiu ya kutosha. Biblia ilisema, mmebarikiwa ninyi mnapokuwa na njaa na kiu ya haki. (Matayo 5:6). Unapokuwa na kiu, unaweza ukanywa. Na kwa kadiri unavyokunywa, ndivyo unavyozidi kukua. Unapata Neema nyingi zaidi, unapata nguvu zaidi, imani nyingi unapata uavyozidi kuendelea kunywa kutoka kwa Kristo ambaye ni chemchemi ya uzima isiyoisha, kunywa, katika hali ya mbegu [12].

Kristo ndani ya moyo ambaye anakubadilisha, anakufanya wewe unakuwa mtu tofauti, kiumbe kipya (2Kor 5:15-17). [13].

Roho Mtakatifu ni nini? Ni Roho wa kristo ndani yako (Warumi 8:9) yule mfariji; huyu ni Roho Mtakatifu (Yohana 14:19-26). “Punde kidogo,” Alisema Yesu” na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mnaniona; kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, na ndani yenu hata mwisho wa dunia. [14].

Kama akienda kwa Baba, Roho Mtakatifu atakuja. Je ni sawa? Maandiko mengine yalisema, “Kama nisipoondoka, mfariji hatakuja; lakini kama nikienda, nitakuja tena na kuwa pamoja nanyi hata ndani yenu”. (Yohana 16:7-11) Ni Mungu pamoja nanyi, Mungu juu yenu kwanza, pamoja nawe ndani ya Kristo, ndani yako ndani ya Roho Mtakatifu:

Huyu ni Roho Mtakatifu yuko kwa sababu hiyo. Ni kwa ajili ya maisha matakafu; anakufanya uache kusengenya, anakufanya uache kucheza karata, kupiga craps, na vitu hivi vyote ambayo unavifanya kwenye kona. Itakufanya uache kufanya mambo hayo yasiyofaa jinsi ufanyavyo. Kuishi bila uaminifu kwa mkeo. Hivyo ndivyo atakavyofanya. Hiyo ni sawa itakufanya uache kuoa mke wa mtu mwingine hiyo ni sawa kabisa. Hivyo ndivyo alivyo. Ni kukufanya wewe uishi maisha matakafu atakufanya wewe uache kuvuta, na kunywa, na kutaka kuwa mtu mkubwa fulani. Ataondoa vitu hivyo ndani yako. Atakushusha ukifanya hivyo. Hivyo ndivyo alivyo Roho Mtakatifu kwa ajili ya nguvu. Kuweka upendo wako kwa vitu vilivyoko juu. (Kolosai 3:1-4) Nia ya Kristo ndani yako (Wafilipi 2:5-8) Huwezi kujisaidia kuona mambo hayo. Unapoyaangalia, unageuza kichwa chako. Hiyo ni sawa. Ni kukufanya wewe.....

Unasema, siwezi kufanya hivyo. oh siwezi kufanya hivyo. hakika huwezi. Lakini Roho Mtakatifu alikuja kwa kusudi hilo hivyo ndivyo alivyofanya alikuja kuvitoa ndani yako, tabia zote za zamani na mambo unayoyafanya kinyume. Kule kusengenya, kujitenga wewe mwenyewe, ukisema” Mungu abarikiwe mimi ni Mmethodist. Sina cha kufanya na watakatifu wale wanaoviringika”. Roho Mtakatifu anakuja kuyaondoa hayo, mbali na wewe. Na Kama una Roho wa Kristo ndani yako, wewe umetoka juu (Yohana 17:6,14). Hivyo wewe ni mgeni hapa. Lakini una asili ya mahali ulipotoka; hicho ndicho ninachojaribu kusema [15].

Leo, ninashangazwa, mara nyingi ninapowauliza watu je wewe ni Mkristo? Wanasema, mimi ni mmethodisti”. “ Je wewe ni Mkristo”- mimi ni mbaptisti, au mimi ni mpresbyterian, au hata mpentekoste, au Pilgrim holiness, au kanisa fulani’

Sasa, hayo yanaweza yakawa sahihi, lakini hilo siyo swali. Swali ni kwamba. “wewe ni Mkristo”? Na huwezi ukawa Mkristo mpaka umempokea Kristo, Kristo ndani yako (Rumi 8:9) [16]

Ndiyo sababu ni kitu cha lazima katika siku ya leo kumpokea Roho Mtakatifu, kwa sababu ndiye anayeishi maisha yako.

Huishi wewe mwenyewe. Ni Kristo ndani yako. Sasa, Baada ya kwamba umempokea Roho Mtakatifu.

Nakama hana nafasi ya kwanza katika maisha yako (Wakolosai 1:18-20) , sasa ukumbuke kwamba, hujapokea Roho mtakatifu kwa sababu kama yuko ndani yako, Ataishi maisha yake. Siyo wewe tena, “wewe umekufa, na uhai wako

umefichwa ndani ya Mungu, kwa Kristo, na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu” (Wakolosai 3:1-4). Sasa hakuna njia ya wewe kuwa mwenyewe hata kidogo, vile ulivyokuwa. [17].

Angalia, Kristo ndani yako inamfanya yeye kuwa kiini cha maisha ya ufunuo. Unaona? Maisha ya Kristo ndani yako yanamfanya kuwa kiini cha ufunuo: Kristo katika Biblia, inaifanya Biblia kuwa ufunuo mkamilifu wa Kristo. Kristo ndani yako inakufanya wewe kuwa ufunuo mkamilifu wa kitu chote. Unaona kile Mungu anachojaribu kufanya?.

Kuzaliwa mara ya pili ni nini basi? Unasema,” Vema, ndugu Branham, kazaliwa mara ya pili ni nini? Ni ufunuo wa Yesu Kristo binafsi kwako. Amina. Unaona? Siyo ulijiunga na kanisa, ulipeana mikono; umefanya kitu tofauti; ulisema kanuni; uliahidi kuishi kwa kanuni fulani; lakini Kristo, Biblia Yeye ni Neno ambalo limefunuliwa kwako. Na haijalishi mtu yoyote anasemaje, kunatokea nini, ni Kristo. Mchungaji, kuhani, yoyote iwavyo ... ni Kristo ndani yako. Huo ni ufunuo ambao Kanisa linajengwa katika huo (Matayo 16:13-20)

Sasa angalia, Mungu anajitambulisha mwenyewe. Hatupaswi kuwafanya watu kuwa waamini Wakristo kwa serikali, bali kwa ufunuo wa Kristo ndani yako kama Mungu alivyokuwa ndani ya Kristo. Kama Mungu alivyokuwa ndani ya Kristo, Kristo ndani yako. Kile Mungu alichotenda ndani ya Kristo, Kristo anakitenda ndani yako. Ishara Mungu alizofanya ndani ya Kristo, Kristo anazifanya ndani yako. Oh, siyo lakupendeza hilo? Oh, jamani nalipenda hilo.

Yesu alisema siku hiyo (siku ya leo)... siku hiyo (wakati ufunuo huu utakapokuwa ukiwekwa wazi) mtajua kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani yangu. Mimi ndani yenu, na ninyi ndani yangu. (Wakati ufunuo utakapofanywa dhahiri). Siku hiyo, n g kwamba Mimi na Baba tu Mmoja. Mimi niko ndani ya Baba, na Baba ndani yangu. Hapo ufunuo utakapokuja, ni mimi ndani yenu na ninyi ndani yangu (Yohana 14:20).

Ni nini hiyo? Siyo wale watu, kile kichwa na mwili vimekuwa kitu kimoja. Ni Mungu akidhihirishwa ndani ya watu wake. Hiyo ndiyo sababu Mume na Mke siyo wawili tena; ni mmoja. Mungu na kanisa lake ni mmoja: Kristo ndani yako, ufunuo mkuu wa Mungu (Utukufu kwa Mungu), hata kulichukua Jina lake. Jina lake ni Yesu, aliyepakwa mafuta. Sababu anaitwa Yesu, Yeye ni mpakwa mafuta.

Na ni mwili wa Kristo uliopakwa mafuta ukithibitishwa, Mungu akidhihirishwa kama ule mwili ulivyokuwa. Na mwili ule ulikomboa miili hii [18].

Lakini kama unataka kutafuta jinsi ulivyomkuu, weka kidole chako ndani ya dimbwi la maji, au ndoo ya maji, halafu toa kidole chako nje na ujaribu kutafuta ni wapi uliweka kidole chako. Wewe sio chochote. Mungu anaweza

akafanya bila ya wewe; anaweza akafanya bila ya mimi, lakini sisi hatuwezi kufanya bila ya Yeye. Lazima tuwe na Yeye; kwa maana Yeye ni uzima; Na Yeye peke yake. Siyo kujua kitabu chake, siyo kujua hiki, au kujua kile, au kujua kanuni, lakini kumjua Yeye ni uzima, kumjua Yeye kama mtu binafsi, Kristo ndani yako, Neno limefanyika mwili ndani yako (Yohana 17:3). Huko ni kumjua Yeye. Wakati wewe na Yeye mnapokuwa mmoja, kama nilivyosema lazima Yeye aje ndani yako: wewe. Mungu na Mtu waje wawe mmoja. Unajijua ulivyo mdogo [19]

Ni Kristo ndani yako, Mungu, akikaa ndani ya moyo wa binadamu [20]

Mkristo? Ni Kristo ndani yako. Na kama Kristo yu ndani yako, hapo sasa Neno liko ndani yako. [21]

Utiifu mkamilifu katika Neno unamleta Mungu, lile Neno la milele ndani yako. [22]

Kama Roho wa Mungu yuko ndani yako, inakufanya uishi kama Kristo. Hapo unakuwa barua iliyokatibiwa, isomwayo na watu wote, Kristo ndani yako, akionyesha Nuru yake hupitia wewe (2Kor. 3:1-3), kama Mungu alivyokuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, na kumuonyesha Mungu kupitia mwili wake mwenyewe (2Kor. 5: 18 – 19). [23]

Sasa watu wengi hawangesoma Biblia. Lakini Mungu amekufanya wewe uwe muwakilishi aliye hai. Wewe ni barua inayotembea, unapaswa kuwa Biblia inayotembea, Kristo ndani yako. Unapaswa kuwa Neno la Mungu linalotembea. Na kama unakiri kwamba wewe ni Mkristo na sivyo hivyo, ushawishi wako kile unachoshawishi kitakufanya ujibu kwa nafsi hiyo uliyoigeza pembeni, mbali na Kristo, katika siku ya hukumu. [24]

Lakini, Oh, kaka, Wakati hiyo ishara imewekwa ndani ya moyo wako, na unajua ni ufufuo wa Yesu Kristo ndani yako, jambo fulani limetokea. Hakuna kitakachokugeza. Unajua wewe ni wa wapi.

Utiifu mkamilifu katika Neno la Mungu unakupa wewe haki ya kupokea ile ishara na hakuna kingine tena. “Amebarikiwa yule ambaye anashika amri zote za Mungu, awe na amri ya kuuendea huo mti wa uzima (ufunuo 22:14 – 15). Sasa hapo chukua Ishara yako, ambayo unajua ambayo ni Kristo ndani yako, ichukue hiyo, ni uhai wa Yesu ndani yako. [25]

Siyo nafsi nyingine iliyotoka kwake iitwayo Roho Mtakatifu, lakini ilikuwa ni Yeye mwenyewe. Unalipata hilo? Yeye mwenyewe akijimwaga ndani ya watu, Kristo ndani yako. Jinsi lilivyo zuri ilivyo ajabu kufikiria, Mungu mwenyewe akijimwaga ndani ya wanadamu, ndani ya waamini, akijimwaga nje. Ilikuwa ni sehemu ya mchezo wake wa kuigiza kufanya hivyo. Mungu utimilifu wake wote; Uungu wote kwa jinsi ya mwili katika utu wa Yesu Kristo (Wakolosai 2: 9 – 10). Alikuwa ni Mungu na ni Mungu pekee, siyo nafsi ya tatu au nafsi ya

pili au nafsi ya kwanza, lakini ni Nafsi ya Mungu akiwa amefunikwa ndani ya mwili wa nyama. [26]

Kwa hiyo mpate Kristo moyoni mwako, Kristo na Roho Mtakatifu ni kitu hicho hicho. Roho Mtakatifu, “Kristo” maana yake “mpakwa mafuta” Na Roho Mtakatifu ni huo upako, na wewe ndiwe ambaye umepakwa mafuta. Unaona? Na ni Kristo ndani yako anayekupaka mafuta. Unaona ninachomaanisha?

Hapo sasa unacho kitu sahihi. Hapo sasa anaweza kukutumia kwa chochote anachotaka kukutumia. Kwa sababu uko katika mwili na unaweza kutumiwa katika karama yoyote. Lakini angalia, kuwa na moja ya hizo karama nje ya mwili, haitakufanyia jambo lolote zuri. “Hata kama ningenena kwa lugha za wanadamu na Malaika, kama sina upendo hainifaidii kitu. Hata kama ningekuwa na Imani na ningeweza kuelewa siri zote za Mungu, hainifaidii kitu. Hata kama niutoe mwili wangu uungue moto kama sadaka, nikitoa mali yangu yote niwape maskini, hata ningekuwa na Imani ya kuhamisha milima, mimi bado sio kitu (1Kor. 13:1 – 3). Unaona? Usitegemee vitu hivyo. Roho Mtakatifu ni kiumbe; Ni Mungu, Mungu ndani yako, Nafsi ya Mungu, ambayo imewasha utu wako wote.

Umebadilishwa, umekuwa kiumbe kipya (Galatia 6:15). Kitu chochote ambacho hakiko sahihi, atakueleza kuwa siyo sahihi, acha, usikifanye. “Baba, sikumaanisha kufanya hivyo, nisamehe mimi”. Unaona? Na huyo ni Roho Mtakatifu. [27]

Tutawezaje kuingia Mbinguni na huku tunasema, vema ninaamini hili, lakini siamini hili? Lazima uwe Neno lote, kwa maana wewe ni sehemu Yake.

Hivyo ndivyo Mungu anavyojaribu kulifanya Kanisa la leo, siyo kwa kanuni. Na wanajaribu kutulazimisha sisi katika hizo. Unaona hiyo inakuja. Yale maandiko kwenye ukuta. Haitakuwa muda mrefu tutakuwa Kanisa la Dunia nzima, na kila Kanisa inabidi kukubaliana na hilo au siyo liwe tayari kusimamia mazingira yoyote? Vema, uko tayari kusimamia hilo? Ni vizuri usifanye hivyo kwa sababu tu ni kitu sahihi. Ni vizuri uwe na Kristo ndani yako, kwa sababu Neno ni la milele na lile Neno ndilo litakalokuinua wewe tena. Uwe sehemu ya hilo Neno. Unatambulishwa na hilo Neno. [28]

Nukuu za kiingereza:

- [1] Uungu wa Yesu Kristo (kitabu cha 20 na 12) Aya 82
- [2] Israeli katika Misri Aya 63 – 66
- [3] Maswali na majibu juu ya chapa ya mnyama C.O.D uk. 159.
- [4] Ushirika ni kwa ukombozi kitabu cha 26 na 17 Aya 244
- [5] Uthibitisho wa kufufuka kwake (kitabu cha 26 na 16) Aya 145
- [6] Ni wapi nafikiri wapentekoste walishindwa (5-1111) Aya 44
- [7] Kwa nini watu wanayumba yumba? (kitabu cha 2 na 14) uk. 18

- [8] Yesu Kristo yule yule (56-0426), Aya 35.
- [9] Muda uliojaribiwa kumbukumbu za Mungu (57-0818), Aya 46
- [10] Waebrania sura 5na6 Uk 189.
- [11] Msikieni Yeye (58-0328), Aya 43.
- [12] Tuonyeshe Baba (56-0419E), Aya 34
- [13] Tangu mwanzo haikuwa hivyo (59-1125), Aya 30
- [14] Roho Mtakatifu ni nini? (kitabu cha 4 na 2), Aya 52,57
- [15] Kwanini tumepewa Roho Mtakatifu kitabu cha 4 na 3, Aya 65, 106, 147.
- [16] Twende kwa nani Aya 16 [17] Ushawishi (63-0803E), Aya 22.
- [18] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa, Uk 36, 65, 85.
- [19] Ushawishi (63-1130B), Aya 113.
- [20] Karama za Mungu siku zote hutafuta mahali pake (kitabu cha 6 na 3), Aya 88.
- [21] Kuna mtu anayeweza kuwasha taa (kitabu cha 6 na 1), Aya 209.
- [22] Ile Ishara(64-0208), Aya 124
- [23] Tunataka kumuona Yesu (57-0226), Aya 21
- [24] Ushawishi (64-0215), Aya 26 [25] Ile ishara (64-0308), Aya 131, 139.
- [26] Kufunuliwa kwa Uungu kitabu cha 9 na 1, Aya 77
- [27] Maswali na majibu (64-0830 M) COD uk 1079
- [28] Kile kipeo cha Mungu kilichotambulishwa (64-1205), Aya 69

Jiwe la kiroho la kujengea no. 144 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69, D – 75328 Schomberg, Germany simu (+49) 7235 -7613, Fax – 3306.

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia. Na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. (Ndg. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho Uk. 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

Charles E.Y. Kanju
Box 5138, Tanga
E-mail: chaelika@Hotmail.com
cellphone: 0784 704299